Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3587

East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 8, Issue 2, 2025
Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

Original Article

Mahusiano ya Uwezo katika Muwala wa Mada katika Hotuba Teule za Marais Kikwete na Samia, Kenya

Sammy Dimbu[1], Prof. John Kobia, PhD[1] na Dkt. Mary Kanyua, PhD[1]*

[1] Chuo Kikuu cha Chuka, S.L.P 109, Chuka, Kenya.
[*] ORCID ID; https://orcid.org/000-0001-5070-6915; Barua pepe ya mawasiliano: dimbuliana@gmail.com

DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3587

Tarehe ya Uchapishaji:

05 Septemba 2025

Istilahi Muhimu:

Diskosi za Kisiasa, Hotuba teule, Muwala, Mada na Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi.

IKISIRI

Muwala huchukuliwa kuwa kipengele cha diskosi ambacho hufasiriwa kulingana na muktadha na hujumuisha dhana zinazohusiana, utathmini na msemezano. Makala hii iliangazia makala muwala wa mada katika hotuba teule za Marais Jakaya Kikwete (Kikwete) na Samia Suluhu (Samia). Nadharia iliyoongoza makala hii ni Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi. Nadharia hii hudokeza kuwa lugha yenyewe haina mamlaka bali huyapata inapotumiwa na wenye mamlaka katika miundo ya kijamii. Sampuli ya makala hii ilipakuliwa kutoka Kumbukumbu za Kudumu za Mabunge ya Kitaifa nchini Kenya zilizoko mtandaoni. Diskosi za hotuba teule zilizo sampuli ya makala hii ni zile zilizowasilishwa kwa lugha ya Kiswahili baina ya miaka (2013-2022). Kipindi hiki ni awamu ya 11 na 12 ya Bunge la Kitaifa na awamu ya 2 na 3 ya Bunge la Seneti nchini Kenya. Jumla ya hotuba 2 ziliteuliwa kimakusudi kwa kujikita kwenye mbinu ya uchanganuzi wa yaliyomo. Muundo wa kimaelezo ulitumika katika kukusanya, kuchambua na kuwasilisha matokeo ya utafiti. Data ya makala hii ilikusanywa kutokana na mchakato wa usomaji wa kina wa hotuba teule. Data iliainishwa kulingana na maswali ya utafiti. Matokeo yalibainisha kuwa vipengele vya kigezo cha hali, washiriki katika diskosi, madhumuni ya mawasiliano, kitendo neni kilichotendwa na kaida za mawasiliano yalikuza muwala wa mada katika hotuba teule. Makala hii ilibainisha namna masuala ya kimuktadha huchangia muwala wa ndani na wa kijumla ili kuleta uelewaji wa diskosi ili kukuza mahusiano ya uwezo katika diskosi. Makala hii ilipendekeza tafiti za baadae zifanywe kuhusu namna vibainishi vya muktadha wa diskosi hukuza maana ya implikecha.

APA CITATION

Dimbu, S., Kobia, J. & Kanyua, M. (2025). Mahusiano ya Uwezo katika Muwala wa Mada katika Hotuba Teule za Marais Kikwete na Samia, Kenya. *East African Journal of Swahili Studies*, *8*(2), 283-294. https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3587

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3587

CHICAGO CITATION

Dimbu, Sammy, John Kobia and Mary Kanyua. 2025. "Mahusiano ya Uwezo katika Muwala wa Mada katika Hotuba Teule za Marais Kikwete na Samia, Kenya". *East African Journal of Swahili Studies* 8 (2), 283-294. https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3587

HARVARD CITATION

Dimbu, S., Kobia, J. & Kanyua, M. (2025) "Mahusiano ya Uwezo katika Muwala wa Mada katika Hotuba Teule za Marais Kikwete na Samia, Kenya", *East African Journal of Swahili Studies*, 8(2), pp. 283-294. doi: 10.37284/jammk.8.2.3587

IEEE CITATION

S., Dimbu, J., Kobia & M., Kanyua "Mahusiano ya Uwezo katika Muwala wa Mada katika Hotuba Teule za Marais Kikwete na Samia, Kenya", *EAJSS*, vol. 8, no. 2, pp. 283-294, Sep. 2025.

MLA CITATION

Dimbu, Sammy, John Kobia & Mary Kanyua. "Mahusiano ya Uwezo katika Muwala wa Mada katika Hotuba Teule za Marais Kikwete na Samia, Kenya". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 8, no. 2, Sep. 2025, pp. 283-294, doi:10.37284/jammk.8.2.3587.

UTANGULIZI

Lengo la makala hii lilikuwa kuchanganua mahusiano ya uwezo katika muwala wa mada katika hotuba teule za Marais Kikwete na Samia katika vikao vya pamoja vya Mabunge ya Kitaifa nchini Kenya. Uchanganuzi faafu wa kutathmini diskosi za kisiasa kiisimu ni uchanganuzi makinifu wa diskosi. Mtazamo huu hujikita kwenye mazoea ya kijamii na athari ya ukosefu wa usawa katika diskosi (Gee, 2014). Aidha, hutathmini upataji na udhibiti wa muktadha, maandishi na mazungumzo na mikakati ya udhibiti wa akili kupitia miundo ya kijamii. Mtazamo huu ulichunguza kimakinifu namna ukosefu wa usawa wa kijamii ulivyowasilishwa, kuashiriwa, kuundwa, na kuhalalishwa kupitia diskosi za hotuba teule katika makala hii. Kwa hivyo, uchanganuzi huu ni ufichuzi wa miundo fiche ya mamlaka kwenye mifumo ya kisiasa, kitamaduni, kijamii na kiitikadi.

Muundomaikro wa muwala wa mada uliangaziwa katika kubainisha kuwa mpangilio wa mada katika hotuba teule haukutokea tu kwa kushtukiza bali uliendeleza mahusiano ya uwezo mbalimbali. Mahusiano ya uwezo yalibainishwa ni nani aliamua ni suala lipi lilikuwa muhimu katika diskosi za hotuba Marais Kikwete na Samia katika Bunge la Kitaifa nchini Kenya. Marais hawa walidhibiti makini ya ajenda ya umma katika hotuba teule. Mahusiano haya yalielekeza namna mada katika hotuba teule zilieleweka. Kwa kuteua na kuangazia vipengele fulani vya suala na kupuuza vingine, Marais hawa walikuza ufasiri mahususi, utoaji wa maelezo, utathmini wa kimaadili, au kutoa masuluhisho. Namna masuala yalivyowasilishwa yalilenga kubadili maoni ya umma na sera, kwa kufichua mamlaka ya wanaodhibiti usimulizi katika hotuba teule. Mahusiano ya uwezo ya Marais Kikwete na Samia au taasisi za kisiasa walizowakilisha zilikuwa na mamlaka ya kuamua ni taarifa zipi zilikuwa muhimu. Kwa kuondoa vipengele fulani vya ukweli au mada Marais Kikwete na Samia walidhibiti uelewaji wa umma wa suala fulani na kudhibiti upaswaji wa taarifa, hivyo kuendeleza nafasi ya mamlaka.

Kuidhinishwa kwa katiba ya mwaka 2010 nchini Kenya kulizua masuala mbalimbali yaliyochochea makala hii. Kwanza, Kiswahili ni lugha rasmi. Marais Kikwete na Samia waliidhinishwa kisheria kutumia lugha ya Kiswahili katika Mabunge ya Kitaifa. Pili, kuundwa kwa chemba mbili: Bunge la Kitaifa na Seneti. Kuwepo kwa Bunge la Kitaifa na la Seneti kuliibua uwezekano wa kufanyika kwa vikao vya pamoja. Pia kuliwezesha kuwepo kwa Kanuni ya Kudumu 25(1) na 26(2) Bunge la Kitaifa na Seneti mtawalia. Kanuni hizi ziliwapa Maspika, Viongozi wa Wengi na Wachache uwezo wa kualika wageni mashuhuri. Kanuni hizi zilihalalisha mchakato wa kuwaalika Marais Kikwete na Samia kuhutubia vikao vya pamoja vya Mabunge nchini Kenya. Kwa mujibu wa Bayley (2004) tafiti zinazohusu bunge zimepuuza kufanya tafiti kuhusu

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3587

diskosi za bunge kiisimu licha ya bunge kuwa taasisi inayozungumza. Makala hii ililenga kufidia pengo hili kwa kuchanganua muwala wa mada katika hotuba za marais kikwete na samia katika vikao vya pamoja vya Mabunge ya Kitaifa, Kenya

MAPITIO YA MAANDISHI

Majukumu ya hotuba kama diskosi iliyoandikwa si tu njia ya kupashana habari bali ni mchakato wa kuendeleza maslahi ya wanasiasa. Mifumo ya kiutawala na michakato ya kiitikadi huwasilishwa kupitia hotuba za kisiasa. Utafiti wa Habwe (1999) uliangazia uchanganuzi wa diskosi katika hotuba za kisiasa zilizowasilishwa kwa lugha ya Kiswahili. Utafiti wa Habwe (keshatajwa) ulijikita katika hotuba nne zilizokusanywa katika Miji ya Nairobi na Mombasa. Hotuba hizi zilizotolewa katika michakato ya kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 1997 nchini Kenya. Utafiti wa Habwe (keshatajwa) ulibainisha kuwa maana ya kipragmatiki katika mada ya hotuba za kisiasa ni mhimili mkuu katika ukuzaji wa muwala katika diskosi za kisiasa. Mahitimisho ni kuwa matumizi ya maswali balagha yalikuwa miundomaikro maarufu iliyotumiwa na wanasiasa kujieleza katika sampuli ya utafiti wake. Makala hii ilizingatia vigezo vya kutathmini muwala wa mada vilivyobainishwa katika utafiti wa Habwe (keshatajwa). Hata hivyo, utafiti wa Habwe (keshatajwa) ni tofauti na huu kwa sababu sampuli ya makala hii ilitokana na hotuba za Marais Kikwete na Samia katika vikao vya pamoja katika Mabunge ya Kitaifa nchini Kenya.

Dontcheza-Navratilova (2010) aliangazia muwala katika hotuba za kisiasa kwa kujikita katika mawazo, mwingiliano wa washiriki wa kijamii na maana ya kimuundo katika hotuba za ufunguzi katika mikutano ya Umoja wa Mataifa. Utafiti wake ulibainisha kuwa vipengele vya muwala katika hotuba hizi kwa kuzingatia muwala na kughilibu, udhibiti wa mada ya diskosi na muundo wa kibalagha, matumizi ya kimkakati ya diskosi na vibainishi vya diskosi. Utafiti wa Dontcheza-Navratilova (keshatajwa) ulifaa makala hii katika kufafanua vipengele vya muwala katika mada na muundo wa diskosi teule. Utathmini wa muwala wa mada uliangaziwa katika kigezo cha hali, washiriki wa kijamii katika diskosi, madhumuni ya mawasiliano, kitendo neni kilichotendwa, na kaida za mawasiliano ulirejelea katika makala hii. Aidha, uchanganuzi wa muundo wa hotuba teule katika sehemu za utangulizi, mjadala na hitimisho ni masuala yaliyoangaziwa katika hotuba teule. Tofauti ni kuwa makala hii haujikiti tu katika miundomaikro ya mada tu bali ulifafanua namna miundomaikro hii ilikuza mahusiano ya uwezo.

MISINGI YA NADHARIA

Nadharia iliyoongoza makala hii ni Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi. Nadharia ya Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi iliasisiwa mwanzo wa mwongo wa 1990 na kundi la wasomi mbalimbali. Hawa ni pamoja na Theo van Leeuwen, Gunter Kress, Teun van Dijk na Norman Fairclough. Uchanganuzi makinifu wa diskosi ni mfumo unaochanganua uhusiano uliopo kati ya diskosi na itikadi. Nadharia hii huchunguza kimakinifu namna ukosefu wa usawa huwasilishwa, huashiria, husheheni na huhalalishwa kupitia lugha. Vilevile, huchangia katika kuonyesha namna muundo wa diskosi huhalalisha na kupinga mahusiano ya uwezo ya kihejemonia katika muktadha wa jamii.

Tafiti zinazoegemezwa katika nadharia ya uchanganuzi makinifu wa diskosi huchukua mitazamo mbalimbali ya kisarufi. Dhana muhimu kama vile diskosi, makinifu, itikadi na mamlaka hutofautiana kulingana na mitazamo hii. Kwa mujibu wa van Dijk (1995) mitazamo ya uwingipande, wingiviwango, wingitaaluma na mwingilianotaaluma hupendekezwa katika uchanganuzi wa diskosi. Uhakiki wowote ule lazima ubainishe mtazamo uliozingatiwa. Ina maana kuwa uchanganuzi makinifu wa diskosi si mfumo funge. Mitazamo ya nadharia hii hufafanua diskosi kuwa mchakato, ung'amuzi, na kumbukumbu za kijamii na kihistoria. Mitazamo hii

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3587

ilitumiwa katika kukusanya data, kuchambua data na kuwasilisha matokeo ya makala hii kutokana na sampuli ya hotuba teule. Mihimi ya nadharia ni Diskosi huangazia changamoto za kijamii, mahusiano ya uwezo hukuzwa na mazoea ya kijamii, diskosi husheheni jamii na utamaduni, diskosi hutekeleza jukumu la kiitikadi, diskosi ni kumbukumbu za kihistoria, kuna uhusiano wa kimwingiliano kati ya usemi na jamii, uchanganuzi wa diskosi ni kutafsiri na kufafanua na diskosi ni aina ya tendo la kijamii

MBINU ZA UTAFITI

Muundo uliochukuliwa katika makala hii ni wa kimaelezo kwa sababu data ya utafiti huu ilichambuliwa kiufasiri. Uchanganuzi wa yaliyomo ulitumika kutambua mada na ruwaza, kisha uchanganuzi wa kiufasiri ukatumika kueleza maana fiche na mahusiano ya uwezo. Hotuba iliyoteuliwa kimakusudi ilikuwa ile iliyotolewa na Rais Kikwete tarehe 6/10/2015 katika kikao kilichoandaliwa kulingana na ilani ya Gazeti la Serikali ya Kenya nambari 7371 na 7372 tarehe 1/10/2015. Isitoshe, hotuba ya Rais Samia tarehe 5/5/2021 iliteuliwa kimakusudi. Hotuba hii ilitolewa katika kikao kilichoandaliwa kwa mujibu wa ilani nambari 4199 na 4200 ya Gazeti la Serikali ya Kenya, tarehe 3/5/2021. Vikao vya pamoja vya mabunge ya kitaifa nchini Kenya kati ya miaka (2013-2022) viliteuliwa kimakusudi.

MATOKEO YA MAKALA

Matokeo ya makala hii ni kuwa miundomaikro ya muwala wa mada na muundo wa hotuba teule ilibainika katika sampuli ya makala hii.

Muwala wa Mada

Muwala ni sifa ya kimsingi ya diskosi. Dhana hii hurejelea mfuatano wa matukio kwa utaratibu kiasi kwamba yanakuwa na mshikamano wa mawazo katika diskosi nzima. Makala hii ilifafanua dhana ya muwala kuwa kipengele cha kisemantiki kinachofasiri ujumbe katika sentensi moja ikilinganishwa na sentensi nyingine katika diskosi nzima ya hotuba teule (Dimbu, 2021). Kwa mujibu wa Crombie (1985) muwala hupatikana kutokana na uhusiano wa kutabirika kwa sentensi na madai yanayoziweka pamoja katika diskosi. Muwala wa mada hutokana na vipengele vya diskosi vinavyohusiana kimada. Masuala ya kuzingatia katika kubainisha muwala unaokuzwa na mada ni namna dhana ya mada ilivyochangia katika uelewaji, muwala wa jumla na wa ndani (Habwe, 1999). Dhana ya mada hufafanua namna sentensi au vifungu vya sentensi mbalimbali katika diskosi hufungamanishwa na kuwa sehemu ya diskosi nzima, ili kutofautisha kifungu kilichohusu “pesa” na vingine vilivyohusu “ngono” au “mchezo” (Habwe, 1999). Tazama hapa chini madondoo ya (1a) na (b) katika hotuba teule ya Rais Kikwete, na (1c) na (d) katika hotuba teule ya Rais Samia ambayo ni sehemu za utangulizi na hitimisho mtawalia:

(1a) Ile hotuba ya Kimombo haitoshi? Mhe. (Mheshimiwa) Justin Muturi, Spika wa Bunge la Kitaifa na Mhe. (Mheshimiwa) Ekwe Ethuru, Spika wa Seneti, Wabunge wa Kenya. Kwangu mimi ni heshima na bahati kubwa, ambayo daima nitaikumbuka na sitawahi kamwe isahau. Nashukuru zaidi kwa kunipa nafasi hii wakati ambapo nimebakisha siku chache kumaliza kipindi changu cha uongozi na nchi yangu, kwa mujibu wa katiba ya nchi yetu. (ukurasa wa 5).

(b) Ninamshukuru Mhe. (Mheshimiwa) Spika wa Bunge la Kitaifa na Spika wa Seneti kwa kunipatia fursa hii ya kuagana nanyi na wananchi wa Kenya kupitia kwenu. Asanteni sana nimesema kwamba nikiwa Rais inakuwa taabu kidogo. Nikija baada ya kuwa Rais sijajua mambo yanakuwaje-nadhani nitapata nafasi zaidi ya kukutana na marafiki wengi kuliko ilivyo hivi sasa. Wakati huo tutakutana. Asanteni (ukurasa wa 11).

(c) Rais Kenyatta ni mtu wa kutimiza ahadi. Mara tu baada ya kumalizika kipindi cha maombolezo, alinitumia ujumbe maalum kuniona, ambao pia

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3587

uliambatana na mwaliko wa kutembelea Kenya. Na mimi nimekuja Kenya kuitika wito wake (ukurasa wa 4).

(d) Natumia fursa hii kwa mara nyingine tena kuwashukuru waheshimiwa Maspika kwa mara nyingine tena kwa kunikaribisha. Lakini namshukuru Rais Uhuru Kenyatta kwa mwaliko wa kuniomba mimi kufanya ziara hii rasmi ya kiserikali nchini Kenya. Nataka niwadhibitishie kwamba tumevuna mengi na makubwa sana katika ziara hii. Ziara hii imefungua milango mingi sana. Lililobaki, mtusimamie kwenye utekelezaji (ukurasa wa 13).

Madondoo ya (1a) na (b) yalitokana na hotuba teule ya Rais Kikwete. Hotuba hii ilihusu masuala ya ushirikiano wa kikanda. Uhusishaji wa madondoo haya ulitokana na maarifa ya awali kuwa Rais Kikwete alikuwa akistaafu baada ya awamu yake ya uongozi kuisha. Kwa mujibu wa Fetzer na Meierkord (2002) aina ya mfumo wa ufasiri wa diskosi kulingana na maarifa fulani huunga mkono mtiririko wa masuala fulani katika diskosi. Suala la kustaafu kwa Rais Kikwete lilijitokeza katika madondoo ya (1a) na (b) yaliyokuwa sehemu ya utangulizi na hitimisho mtawalia. Muwala wa mada katika hotuba teule ulirejelea kiwango kilichozingatia mada mahususi au seti ya mada zilizohusiana.

Kwa mujibu wa Daneš (1995) maendeleo ya usemi kuanzia utangulizi hadi hitimisho hufanikishwa kupitia kutegemeana kimaudhui na maarifa mapya yanayohusiana kwa uwazi katika sentensi kimada. Dhana ya mada kati ya madondoo ya (1a) na (b) ilizingatiwa kutokana na yaliyomo. Ingawa madondoo haya hayako katika uhusiano wa ujirani, yaliyomo yalihusu mada kuu ya hotuba teule. Kinachoendelea katika madondoo ya (1a) na (b) kilipangiliwa kulingana na upeo wa shughuli na mada. Shughuli yenyewe ilikuwa kitendo cha Rais Kikwete kutoa hotuba teule. Kulingana na Dontcheza-Navratilova (2010), uchanganuzi wa muundo wa ujumbe katika kutathmini muwala wa diskosi unazingatia habari inayoeleweka na washiriki wa kijamii katika diskosi. Mada katika madondoo ya (1a) na (b) ilikuwa kustaafu kwa Rais Kikwete baada ya kukamilika kwa awamu yake ya uongozi.

Kulingana na Firbas (1992) habari mpya zilizopeanwa katika sehemu ya utangulizi huendelezwa katika sehemu zinazofuata za usemi, utofauti wa mada hutokana na mtazamo wa jukumu la kiuamilifu wa sentensi. Ingawa madondoo ya (1a) na (b) hayafuatani moja kwa moja, mahusiano ya kimuwala yalitokana na mfumo wa ukisiaji wa maarifa ya awali. Maarifa haya hayakuongozwa na matumizi ya vipengele vya mshikamano katika diskosi. Kwa mujibu wa van Dijk na Kintsch (1983) ufahamu wa diskosi hutegemea uchukulio wa mikakati ya kidiskosi katika kuunda wingiviwango vya kiakili; msingi wa ufahamu huu ni vipengele vya kiisimu, maarifa ya awali, imani na malengo ya washiriki katika mtagusano. Ukisiaji wa uhusiano wa mada katika madondoo (1a) na (b) ni mchakato wa kutimiza mahusiano ya kimantiki kwa kutumia kipengele cha muundomakro wa muwala wa jumla.

Kwa mujibu wa Mcleod na Paradis (2024) uchanganuzi makinifu wa diskosi huangazia muktadha wa lugha. Muktadha husheheni utambulisho wa kijamii wa hadhira, usuli wa kihistoria na kitamaduni na muundo mpana wa mahusiano ya uwezo. Muktadha ni muhimu katika upataji wa muwala wa kijumla katika madondoo ya (1a) na (b). Kwa mujibu wa Givón (1995) muwala hukuzwa na muktadha wa mahusiano ya kiwakati kati ya washiriki katika diskosi. Hali hii hufanikishwa kupitia urejeleaji wa kibinafsi wa washiriki na deiksisi za mahali na wakati kutokana na mtazamo wa usemi katika diskosi husika. Kwa mujibu wa Fairclough (2013) uchanganuzi wa muktadha hutegemea kitendo kinachoendelea, washiriki, uhusiano wa masuala na jukumu la lugha katika kile kinachoendelea. Tazama hapa chini vipengele vilivyokuza muwala kati ya madondoo ya (1a) na (b):

Kigezo cha Hali

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3587

i. Mandhari: Hotuba hii ni diskosi ya Bunge na ilitokea katika vikao vya pamoja vya Mabunge ya Kitaifa nchini Kenya. Rais Kikwete na hadhira walikuwa na uhusiano wa kijukumu wa pamoja. Uhusiano huu ulitokana na ukweli kuwa wote walikuwa wanasiasa.

ii. Eneo la tukio: Rais Kikwete alitumia jukwaa la Bunge la Kitaifa nchini Kenya kufafanua misimamo ya kiitikadi, kitaasisi, kitamaduni na kisaikolojia ili kubainisha turathi za pamoja na hadhira lengwa. Kwa mujibu wa Hunston & Thompson (2000) utathmini wa diskosi husawiri maoni yanayodhihirisha turathi inayohusiana na itikadi ya jamii. Lugha katika hotuba teule si bia bali ilikuwa mwangwi wa kuendeleza miundo ya kijamii iliyopo ya mamlaka katika jamii.

iii. Kikoa; madondoo ya (1a) na (b) yalikuwa sehemu ya hotuba ya Rais Kikwete kuhusu masuala mbalimbali; utathmini wa uangaziaji wa dhana, watu, matendo na matukio kwa kushinikiza au kulalama kuhusu masuala mbalimbali yaliyohusu uhusiano wa kidiplomasia katika kipindi mahususi cha kihistoria. Aidha, kudhihirisha ujitoleaji wa Rais Kikwete kukuza uhusiano uliopo kati ya Mataifa ya Kenya na Tanzania.

iv. Sehemu iliyoangaziwa; ushirikiano wa nchi za Kenya na Tanzania katika ulingo wa sekta mbalimbali za mahusiano. Hotuba teule iliwakilisha maono ya Rais Kikwete kuhusu uhusiano uliopo kati ya mataifa haya. Kwa mujibu wa Mcleod na Paradis (2024) kwa kuangazia hotuba za kisiasa uchanganuzi makinifu wa diskosi hutambua turathi za kitamaduni na mikakati ya mamlaka. Aidha, Rais Kikwete alitumia lugha ya kipekee kuwasilisha imani na turathi za kundi tawala. Lugha hii ilihusishwa na tamaduni, ambayo ilisheheni siasa katika jamii ya hadhira lengwa.

Washiriki wa kijamii katika Diskosi

i. Utambulisho wa washiriki wa kijamii katika uzalishaji wa hotuba teule ulibainika kutokana na mahusiano ya uwezo baina yao. Mhutubu alikuwa Rais Kikwete. Hadhira lengwa ni Maspika wa Bunge la Seneti, la Kitaifa, wabunge wa Bunge la Seneti na la Kitaifa, wageni waalikwa na hadhira iliyofuatilia hotuba hii kupitia vyombo vya habari.

ii. Uwepo wa hadhira ambayo haikubainishwa, yaani wageni waalikwa. Mheshimiwa Raila Odinga alitajwa si kwa ajili ya kutambuliwa, bali kwa madhumuni ya kuhalalisha nafasi ya Rais Kikwete kama mpatanishi wa mzozo wa kisiasa baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2007.

iii. Majukumu ya kijamii ya washiriki; uhusiano usio sawa kati ya washiriki ulibainika kutokana na taasisi ya bunge. Kulingana na Fairclough (2013) nadharia ya uchanganuzi makinifu wa diskosi hufichua mikakati ya mamlaka na ukosefu wa usawa katika jamii ambayo ni muhimu katika kuangazia changamoto za jamii na kuleta mageuzi ya kijamii. Rais Kikwete alikuwa na mamlaka ya uwezo ya kuhutubia bunge kama Rais wa Tanzania na kuwepo kwa sera na kanuni mbalimbali zilizoongoza vikao vya pamoja vya Mabunge ya Kitaifa nchini Kenya. Hii ni kwa sababu Siasa ni sera zinazohimizwa kupitia mamlaka ya sheria za kitaasisi. Aidha, Spika wa Bunge la Kitaifa alikuwa na mamlaka ya kuendesha kikao hiki kuliko washiriki wengine.

iv. Kiwango cha maarifa ya pamoja: Kiwango cha juu cha maarifa kuhusu uhusiano wa Kenya na Tanzania yaliyowasilishwa na Rais Kikwete. Aidha, kiwango cha chini cha maarifa kuhusu uhusiano wa Kenya na Tanzania wa sehemu ya hadhira lengwa.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3587

Hawakuhusika moja kwa moja na suala la uhusiano wa kidiplomasia. Rais Kikwete alitumia maarifa yake kuhusu uhusiano wa kidiplomasia kughilibu hadhira ili kukubaliana na alichosema. Lugha huathiri jamii kwa kudhibiti diskosi. Rais Kikwete alikuwa na uwezo wa kudhibiti namna hadhira ilivyofikiria kuhusu masuala katika hotuba teule kupitia uwasilishaji wake.

Madhumuni ya Mawasiliano

i. Ukuzaji wa mahusiano ya kijamii: kama vile tambiko za kutoa shukrani. Kwa mfano matumizi ya maneno “Nashukuru” na “Ninamshukuru” katika mifano ya 1(a) na 1(b) mtawalia. Mahusiano ya kijamii yalikuwa sehemu ya uhusiano kati ya makundi ya kijamii na taasisi ya bunge katika vikao vya pamoja vya Mabunge ya Kitaifa nchini Kenya.

ii. Kuhimiza umuhimu wa hotuba teule kwa mtazamo wa sera ya nchi ya Tanzania kuichukulia Kenya kuwa rafiki wa kimkakati.

iii. Utathmini wa washiriki katika kuzalisha hotuba teule kwa kuzingatia mitazamo ya wabunge wa Taifa la Kenya kuhusu uhusiano wa kidiplomasia kati ya mataifa haya na ndio kiini cha kualikwa kuhutubia bunge.

iv. Uhimizaji wa hadhira lengwa kuunga mkono Rais Kikwete katika kuhutubia vikao vya pamoja vya Bunge la Kitaifa nchini Kenya. Hotuba teule ilishinikiza mielekeo, mitazamo na maarifa ya hadhira. Ilitazamia kuathiri ujitambulishaji na itikadi ya hadhira ili kuleta mageuzi katika sekta mbalimbali za kijamii.

v. Utambuaji wa changamoto na kutoa suluhu kwa masuala mbalimbali yaliyokumba mataifa ya Kenya na Tanzania katika ulingo wa kidiplomasia kama vile kupambana na wahalifu, kujenga miundombinu ya pamoja, ushirikiano wa kibiashara na kustaafu kwa Rais Kikwete.

Kitendo neni kilichotendwa

i. Rais Kikwete alihutubu kwa njia ya kimonolojia. Uchanganuzi wa kiutathmini wa muwala huwezesha diskosi za kimonolojia kuwa zenye mtagusano kati ya washiriki wa kijamii katika kuzalisha hotuba teule ili kufanikisha jukumu lake la mawasiliano.

ii. Mielekeo ya washiriki kuhusu diskosi na ujumbe: Hotuba teule iliafikia kigezo cha kuwa kweli, kukubalika na ya dhamana. Hadhira ilishangilia na kujibu maswali. Hii ilikuwa ishara ya kukubaliana na kilichosemwa.

Kaida za Mawasiliano

i. Njia ya uwasilishaji: Hotuba teule ni diskosi ya kimonolojia iliyowasilishwa kwa njia ya mazungumzo na kuchapishwa katika Kumbukumbu za Kudumu za Bunge la kitaifa nchini Kenya.

ii. Kiwango cha kutagusana: kulikuwa na kiwango fulani cha hadhira kushiriki katika uwasilishaji wa hotuba teule kama vile kucheka na kujibu swali.

iii. Uzingatiaji wa kaida za kitaasisi za bunge katika kutagusana na kufasiri; uzalishaji wa diskosi ulilingana na kaida za uzalishaji wa hotuba za bunge. Yaani, ulifuata sheria zilizotawala vikao vya pamoja vya Mabunge. Kikao hiki kilifunguliwa na kufungwa rasmi na Spika wa Bunge la Kitaifa kama ilivyokaida ya sheria za bunge. Nadharia ya uchanganuzi wa diskosi huchunguza aina ya usemi na kaida zake na malengo ya kimawasiliano. Kwa mfano uchanganuzi wa namna hotuba teule zilizingatia kaida za hotuba za kisiasa.

(Dontcheza-Navratilova, 2009: 15)

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3587

Kwa mujibu wa Mcleod na Paradis (2024) uchanganuzi makinifu wa diskosi huchanganua namna muundo wa usemi, kama vile mpangilio, mtiririko na vipengele vinavyokuzana, na namna vipengele hivi huunda shinikizo fulani au usimulizi. Muwala wa jumla kati ya madondoo ya (1a) na (b) ulikuzwa kutokana na hotuba iliyotolewa na Rais Kikwete akitarajia kustaafu kwake. Muwala wa diskosi huathiriwa na mshikamano na mwingiliano wa yaliyomo unaokuza mada kuu ya diskosi (Daneš, 1974). Muwala wa mada ulikuzwa na uhusiano wa kimaana kati ya dhana zilizomo katika madondoo ya (1a) na (b). Yaani, namna kauli binafsi, hoja na sehemu ya hotuba teule zilivyoshikamana na kuchangia katika mada kuu au lengo. Kwa mujibu wa Daneš (1995) muwala wa mada hutokana na uhusiano wa propozisheni katika kiwango cha muundomakro. Madondoo ya (1a) na (b) yanaunganishwa pamoja na ukweli kwamba yalikuwa sehemu ya hotuba teule zilizowahusu Rais Kikwete, hadhira lengwa na Maspika. Hii si kuhusu uthabiti wa kimantiki bali kuhusu jinsi hadhira lengwa ilivyoona umuhimu na madhumuni ya mawasiliano katika hotuba teule.

Madondoo ya (1a) na (b) yalibainisha kuwa Rais Kikwete alihakikisha kuwa yote yaliyoangaziwa katika hotuba teule yalitimiza kigezo cha umuhimu ili kuafikia matakwa ya kiisimu na kimuktadha. Kila sentensi ilikuza mada na kupanua mipaka ya mada. Kwa mujibu wa Fairclough (2013) uchanganuzi makinifu wa diskosi hurejelea muktadha wa kijamii ulioizalisha na kuipokea diskosi kwani muktadha huathiri namna usemi hueleweka. Kustaafu kwa Rais Kikwete katika madondoo ya (1a) na (b) ilikuwa mada kulingana na muktadha ulimotolewa. Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi huangazia matumizi ya lugha kulingana na mtazamo wa kijamii. Lugha haitumiki katika ombwe, bali huathiri na huathiriwa na utamaduni wa jamii. Dhana ya kustaafu ilikuza muwala wa kijumla kwa sababu Rais Kikwete alikuwa akihudumu muhula wa mwisho wa uongozi wa awamu ya nne kwa mujibu wa katiba ya nchi ya Tanzania. Madondoo ya (1a) na (b) yalikamilishana kimada (Gundel na Fretheim, 2006), na kukuza muwala kwa mkabala wa kimawazo.

Kwa mujibu wa van Dijk (1996) mamlaka ni sehemu ya mahusiano kati ya makundi ya kijamii na taasisi. Madondoo ya (1a) na (b) hayakukuza muwala tu bali yaliendeleza mahusiano ya uwezo. Istilahi “nashukuru” na “ninamshukuru” ziliendeleza mahusiano ya uwezo kati ya Rais Kikwete na hadhira lengwa. Mahusiano haya yaliathiri pakubwa namna muwala wa mada ulivyoanzishwa, kudumishwa, na wakati mwingine kuvurugwa kimakusudi katika hotuba teule. Kwa mujibu wa van Dijk (2015) nguvu za hejemonia hudhihirika kupitia kushawishi ili kuficha nguvu za kundi tawala. Yalishawishi hadhira kukubali mhutubu kuwa mwanakundi katika mchakato wa kuibua utambulisho wa pamoja.

Ingawa Rais Kikwete alikuwa akitarajiwa kustaafu baada ya Uchaguzi Mkuu wa 2015, bado alikuwa na mamlaka sawa na Rais Uhuru ndio sababu alialikwa kuhutubia Bunge la Kitaifa kama Rais wa Jamhuri ya Tanzania. Baadhi ya mafanikio yake kwa nchi ya Kenya ni kuwa mpatanishi katika mzozo wa kisiasa wa baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2007 na ujenzi wa miundombinu kama vile barabara ya pamoja. Hata hivyo, alidokeza katika dondoo la (1b) kuwa kustaafu kwake kungemweka katika nafasi sawa ya mahusiano ya uwezo na hadhira. Aidha, alionekana kulaumu itifaki iliyoandamana na ofisi ya Urais kwa kumnyima nafasi ya kutangamana na hadhira. Huu ni mkakati wa kujisifunafsi, yaani alikuwa tayari kutangamana na aliowarejelea kuwa marafiki lakini itifaki iliyoandamana na hadhi ya urais ndio ilimzuia.

Kwa mujibu wa van Dijk (2001), nguvu za ushawishi hutokana na maarifa, habari na mamlaka. Mchakato wa diskosi ni mfumo muhimu wa kijamii unaowasilisha utambulisho kupitia mazoea ya kijamii. Kutokana na kushawishi huku Rais Kikwete alikuwa na haki ya kudai umoja kwa matarajio kuwa hadhira ingekumbatia sera za

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3587

serikali ya Tanzania ya wakati huo kuhusu uhusiano uliopo na nchi ya Kenya. Kwa mujibu wa Fairclough (1992) wanasiasa hutumia itikadi ili kuzua hali ya ukosefu wa usawa ili iwe rahisi kupata mamlaka. Mahusiano ya uwezo kati ya Rais Kikwete na hadhira lengwa yalifungamana sana na itikadi yake kuhusu mtazamo wake kuhusu uhusiano uliokuwepo kati ya Kenya na Tanzania. Yalifungamana na itikadi tawala iliyojikita katika sehemu ya mjadala kiasi kwamba mada husika na jinsi ilivyowasilishwa ilionekana kuwa ya kawaida au isiyoweza kuepukika. Huku kuasiliwa kwa mamlaka kulifanya iwe vigumu kupinga machukulio fiche na hivyo muwala wa mada ulijengwa nayo.

Kuighilibu hadhira kupitia Istilahi za "nashukuru" na "ninamshukuru" zilishawishi hadhira kukubali mtazamo wa Rais Kikwete. Vipengele hivi vya kiisimu na kibalagha viliathiri imani au tabia ya hadhira, ama viliimarisha imani na tabia za wale ambao tayari walikubaliana naye kuhusu uhusiano huu. Mkakati wa kushawishi ulichangia katika kukuza muwala katika madondoo ya (1a) na (b) kwa kubainisha mielekeo ya pamoja kati ya washiriki katika uzalishaji wa hotuba teule ili kuendeleza makini ya hadhira kuhusu hotuba teule. Vipengele vilivyobainisha muwala wa kijumla kati ya madondoo ya (1a) na (b) ni mhutubu, lugha, wakati wa kuhutubia, mahali pa kuhutubia, hadhira, uhusiano uliopo kati ya mhutubu na hadhira na mada.

Aidha, muwala hurejelea namna mawazo, mjadala, na hoja zinavyopangwa kwa mantiki na kuwasilishwa kwa namna inayoeleweka (Dontcheza-Navratilova, 2010). Madondoo ya (1c) na (d) yalikuza muwala wa mada licha ya kutokuwa katika sehemu ya ujirani katika hotuba teule ya Rais Samia. Kwa mujibu wa Givón (2001) maendeleo ya kinachokisiwa, mipaka ya matendo, wakati na mahali hubainishwa katika usemi na huwezeshwa na mahusiano ya vipengele vya mwingiliano wa diskosi. Vipengele hivi huongoza ufasiri kwa kujenga muwala wa uwakilishi wa kiung'amuzi wa usemi, ambao huathiriwa na utamaduni, diskosi na maarifa ya pamoja ya hadhira mahususi.

Masuala ya kimuktadha wa kihali yaliyozua muwala wa mada kati ya madondoo ya (1c) na (1d) ni mada iliyohusu mwaliko wa Rais Samia na Bwana Uhuru, Rais wa Kenya wakati huo. Urudiaji wa mada hii uliiimarisha na ilihakikisha ilisalia muhimu akilini mwa hadhira lengwa, hasa kwa washiriki wa jamii katika utoaji wa diskosi teule ambao walikuwa na uwezo mkubwa wa kufikia majukwaa ya kurudia jumbe zao. Aidha, kikao kilichohutubiwa na Rais Samia kiliitishwa na Maspika wa Mabunge ya kitaifa nchini Kenya na hadhira walikuwa wabunge, wageni waalikwa na waliofuatilia hotuba teule kwa vyombo vya habari. Vipengele vingine ni pamoja na nomino, sentensi na vishazi ambavyo vilihusiana kimada katika hotuba teule.

Ingawa madondoo ya (1c) na (1d) yaliunganishwa na vipengele vya mwingiliano na sehemu tofauti za diskosi ilibainika kuwa vipengele vyake vilihusiana kwa kuangazia mwaliko wa Rais Samia na Rais Uhuru. Kwa mujibu wa Miššíková (2007) muwala huwawezesha wanaounga itikadi mbalimbali kushinikiza wengine ufasiri wa ulimwengu na kushawishi hadhira kukubali uelewaji wao wa uhalisia. Mwaliko huu ulikisia na kukuza muwala wa kijumla kwa hadhira kuwa Rais Samia alikuwa na mamlaka sawa na Rais Uhuru. Walikuwa Marais wa nchi ya Kenya na Tanzania mtawalia. Rais Samia aliapishwa baada ya kifo cha Hayati Magufuli, aliyekuwa Rais wa kipindi hicho.

Kwa mujibu wa Sperber na Wilson (2010) mhutubu huafikia kuelewa na kufanya hadhira kufikiria au kutenda kulingana na kile kilieleweka, ingawa hadhira inaweza kupata ujumbe bila kukubali au kuamini kinachosemwa. Kupitia madondoo haya Rais Samia alisawiri sifa ya Rais Uhuru kuwa mwenye kutimiza ahadi. Hata hivyo, haimaanishi kuwa Rais Uhuru alitimiza ahadi zote alizoahidi akiwa Rais. Huu ulikuwa mkakati wa uwakilishaji chanya wa Rais Uhuru ambaye alikuwa mwenyeji

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3587

ili Rais Samia kuwa sehemu ya "sisi". Hadhira haikumtarajia Rais Samia amwakilishe Rais uhuru kwa nafasi hasi. Madondoo ya (1c) na (d) yalifafanua utambulisho wa ndani ya kikundi na nje ya kikundi. Hii iliathiri mada katika madondoo haya ionekane kuwa muhimu au halali kujadiliwa na kundi lililomwunga mkono Rais Uhuru na kuunda muwala wa ndani wa diskosi.

Katika mahusiano ya uwezo Marais Samia na Uhuru walikuwa na nguvu sawa za mamlaka na walikuwa na mamlaka kuliko hadhira kwa ujumla. Hata hivyo, katika muktadha wa mtagusano katika utoaji wa hotuba teule Waheshimiwa Maspika wa Mabunge ya Kitaifa walikuwa na mamlaka kuliko Rais Samia. Wao ndio walioendesha shughuli za kikao siku hiyo. Rais Uhuru kwa kumwalika Rais Samia kulidhihirisha kuwa alikuwa na mamlaka kumliko kwa sababu hangejialika nchini Kenya lakini katika mazungumzo, walizungumza kama washiriki wenye nguvu sawa za kimamlaka. Kila mmoja aliwakilisha maslahi ya nchi yake.

Ingawa mpangilio wa yaliyomo kwa msingi wa mada katika diskosi ni kwa mujibu wa aina ya diskosi (Fries, 1995), muwala katika hotuba teule ulitokana na mkakati wa kibalagha. Mpangilio wa mada ulikuza muwala wa ndani ambao haukuwa wa moja kwa moja. Madondoo ya (1a) na (b), (c) na (d) yalibainisha kuwa muwala wa mada uliletwa na mpangilio wa yaliyomo yaliyotangulizwa, yakajadiliwa na yakakubalika na waliotagusana. Muwala wa mada katika hotuba teule haukuwa tu suala la kiisimu, bali yalikuwa matokeo yaliyobadilikabadilika ya mapambano ya mamlaka.

Marais Kikwete na Samia waliokuwa na mamlaka zaidi na waliweza kuunda, kudumisha, na hata kuvuruga kimkakati muwala wa mada ili kufikia malengo yao ya kisiasa katika hotuba teule. Muwala wa mada ulihusishwa na mada, deiksisi, matendo, na washiriki wa kijamii katika kuzalisha hotuba teule. Kwa mujibu wa Gernsbacher (1997) ufafanuzi wa muwala katika ufasiri wake husheheni hatua tatu: kujenga msingi, na kuweka maarifa kwa msingi wa kujenga muundo mpya. Hivyo, mtazamo wa kiung'amuzi wa ufasiri wa diskosi ni kuwa muwala ni kupata uhusiano kati ya dhana zilizoko katika usemi na hutokana na makisio.

HITIMISHO

Makala hii ilibainisha kuwa vigezo vya muktadha wa hali vya hali, washiriki katika diskosi, madhumuni ya mawasiliano, kitendo neni kilichotendwa na kaida za mawasiliano yalikuza muwala wa mada katika hotuba teule. Makala hii ilibainisha namna masuala ya kimuktadha huchangia muwala wa ndani na wa kijumla ili kuleta uelewaji wa diskosi ili kukuza mahusiano ya uwezo katika diskosi. Yaani mpangilio wa miundomakro katika hotuba teule haikutokea kibahati bali kwa mpangilio maalumu. Mada zilizoangaziwa na Marais Kikwete na Samia katika hotuba teule katika vikao vya pamoja vya Mabunge ya Kitaifa nchini Kenya zilihusu mataifa ya Kenya na Tanzania. Hivyo, ziliendeleza jukumu la bunge la kidiplomasia lililoshirikisha ujihusishaji wake na mambo ya nje ya nchi. Kwa msingi diplomasia ya kibunge ilikamilisha taasisi ya serikali ya utendaji katika sera za kigeni za nchi husika.

MAREJELEO

Bayley, P. (2004). *Cross-cultural Perspectives on Parliamentary Discourse*. John Benjamins Publishing Company.

Crombie, M. A. (1985). *Rhetoric and Coherence: A Case for a Model of Linguistic Interaction*. Croom Helm.

Daneš, F. (Ed.). (1974). *Papers on Functional Sentence Perspective*. Academia.

Daneš, F, (1995). Paragraph – A Central Unit Of The Thematic And Compositional Build-Up of Texts. In: Warwick, B., Tanskanen, S.K., Hiltunen, R. (eds). *Organization in Discourse. Proceedings from the Turku Conference*. Turku: University of Turku.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3587

Dimbu, S. L. (2021). Uchanganuzi Makinifu wa Diskosi katika Vikatuni vya Shujaaz [Master's thesis]. Chuka University Repository. http://repository.chuka.ac.ke/handle/chuka/13938.

Dontcheva-Navratilova, O. (2009). Building up discourse coherence: Creating identities in political speeches.‟ In: Dontcheva-Navratilova, O., Povolná, R. (eds) *Coherence and Cohesion in Spoken and Written Discourse*. Newcastle upon Tyne: Cambridge Scholars Publishing. 97-119.

Dontcheza-Navratilova, O. (2010). *Coherence in Political Speeches: Interpreting Ideational, Interpersonal and Textual Speeches Meaning in Opening Addresses*. Masarykova Univerzita Filozoficka Fakulta.

Fairclough, N. (2013). *Language and Power*. (2nd Ed.). Harlow: Routledge.

Fetzer, A., & Meierkord, C. (Eds.). (2002). *Rethinking Sequentiality: Linguistics Meets Conversational Interaction*. John Benjamins.

Firbas, J. (1992). *Functional Sentence Perspective in Written and Spoken Communication*. Cambridge University Press.

Fries, P. H. (1995). Themes, Methods of Development, and Texts. In R. Hasan & P. H. Fries (Eds.), *On Subject and Theme: A Discourse Functional Perspective* (pp. 317–360). John Benjamins Publishing Company.

Gee, P. J. (2014). *An Introduction to Discourse Analysis: Theory and Method*, Routledge.

Gernsbacher, M. A. (1997). Coherence Cues Mapping During Comprehension. In J. Costermans & M. Fayol (Eds.), *Processing Interclausal Relationships in the Production and Comprehension of Text* (pp. 3–21). Lawrence Erlbaum Associates.

Givón, T. (1995). Coherence In Text Vs Coherence In Mind. In: Gernsbacher, M. A., Givón, T. (eds) *Coherence in Sponateous Text*. Amsterdam, Philadelphia: John Benjamins. 59-116.

Givón, T. (2001). *Syntax: An Introduction (Vol. I & II)*. John Benjamins.

Habwe, H. (1999). Discourse Analysis of Swahili Political Speeches, (Unpublished PhD Thesis). University of Nairobi.

Hunston, S., na Thompson, G. (2000). Evaluation: An introduction. In: Hunston, S., Thompson, G. (eds), *Evaluation in Text. Authorial Stance and the Construction of Discourse*. Oxford: Oxford University Press. 1-27.

Mcleod, N. J., & Paradis, E. (2024). A Meta-Study Analysing the Discourses of Discourse Analysis in Health Professions Education. *Medical Education*.

Miššíková, G. (2007). *Analysing Translation as Text and Discourse*. Praha: JTP.

Sperber, D., & Wilson, D. (2010). A Relevance-Theoretic Approach to the Development of Understanding of Others' Mental States. In E. V. Clark & V. Evans (Eds.), *The Oxford Handbook of Cognitive Linguistics* (pp. 673-693). Oxford University Press.

van Dijk, T. A., & Kintisch, W. (1983). *Stragegies of Discourse Comprehension*. Academic Press.

van Dijk, T. A., (1995). Aim of Critical Discourse Analysis, *Japanese Discourse Journal*, 1(1), pp. 17-28.

van Dijk, T. A., (2001). Critical Discourse Analysis, in: D. Schiffrin, D. Tannen and H.E. Hamilton (eds) *Handbook of Discourse Analysis*. Oxford Press.

van Dijk, T. A. (2015). Critical Discourse Analysis. In D. Tannen, H. E. Hamilton, & D. Schiffrin

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.8.2.3587

(Eds.), *The Handbook of Discourse Analysis* (2nd ed., pp. 466–485). Wiley-Blackwell.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.